Kuwa Mwangalifu Na Marafiki Waovu

(Beware Of Evil Companions)

Na

Ellis P. Forsman

Kuwa Mwangalifu Na Marafiki Waovu

Na

Ellis P. Forsman

Octoba 11, 2011

Kuwa Mwangalifu Na Marafiki Waovu

Mith. 1:10-19

Tunaposoma Mithali, tunaona kwamba hekima inahitaji…

Kumuogopa Mungu, ili kwamba tusikilize Neno lake. Mith. 1:7, "*Kumcha BWANA ni cahnzo cha maarifa. Bali wapumbavu hudharau hekima na adabu.*"

Kuwaheshimu wazazi wetu, ili kusikiliza ushauri wao. Mith. 1:8-9, "*Mwanangu yasikilize mafundisho ya baba yako, wala usiiache sheria ya mama yako, kwa maana hayo yatakuwa kilemba cha neema kichwani pako, na mikufu shingoni mwako.*"

Vipi kuhusu marafiki zetu? Wenzi wetu ambao tunatumia muda mwingi kuwa nao?

Je wanaweza kuwa chanzo cha ushauri mzuri, hekima? Hakika wanaweza.

Mith. 27:9, "*Marhamu na manukato huufurahisha moyo; kadhalika utamu wa rafiki ya mtu utokao katika kusudi la moyo wake.*"

Lakini marafiki fulani wabaya lazima waepukike. Hii inaelezwa katika kifungu chetu cha maandiko.

Mith. 1:10-19, "*Mwanangu wenye dhambi wakikushawishi, wewe usikubali. Wakisema haya! njoo pamoja nasi, na tuvizie ili kumwaga damu; tumwotee asiye na hatia, bila sababu; tuwameze hai kama kuzimu, na wazima kama wao washukao shimoni. Tutapata mali yote ya thamani, tutazijaza nyumba zetu mateka. Wewe utashirikiana nasi, tutakuwa na vitu vyote shirika. Mwanangu, usiende njiani pamoja nao; uzuie mguu wako usiende katika mapito yao. Maana miguu yao huenda mbio maovuni, nao hufanya haraka ili kumwaga damu. Kwa kuwa mtego hutegwa bure, mbele ya macho ya ndege ye yote. Na hao hujiotea damu yao wenyewe, hujinyemelea nafsi zao wenyewe. Ndivyo zilivyo njia za kila mwenye tamaa ya mali; huuondoa uhai wao walio nayo.*"

Ambayo hujumuisha…

Maonyo Ya Baba Kuhusu Marafiki Waovu

Usikubali kujiingiza katika shauri lao

Ushauri wa baba: Mith. 1:10, "*Mwanangu mwenye dhambi wakikushawishi, wewe usikubali.*"

Hasa wanapotafuta kukufanya ili utende uovu. Mith. 1:11-12, "*Wakisema haya njoo pamoja nasi, na tuvizie ili kumwaga damu; tumwotee asiye na hatia, bila sababu; tuwameze hai kama kuzimu, na wazima kama wao washukao shimoni.*"

Wanapokujaribu kwa ahadi za kupata vitu rahisi. Mith. 1:13-14, "*Tutapata mali yote ya thamani, tutazijaza nyumba zetu mateka. Wewe utashirikiana nasi; tutakuwa na vitu vyote shirika.*"

Mfano ni kuingizwa katika mauaji na ujambazi.

Usitembee pamoja nao. Kaa mbali na "marafiki" walio na haraka katika kutenda maovu.

Mith. 1:15-16, "*Mwanangu usiende njiani pamoja nao, uzuie mguu wako usiende katika mapito yao. Maana miguu yao huenda mbio maovuni, nao hufanya haraka ili kumwaga damu.*"

Juhudi zao hakika zitakuwa za bure. Mith. 1:17, "*Kwa kuwa mtego hutegwa bure mbele ya macho ya ndege ye yote.*"

Mara watalipia na uhai wao wenyewe. Mith. 1:18-19, "*Na hao hujiotea damu yao wenyewe, hujinyemelea nafsi zao wenyewe. Ndivyo zilivyo njia za kila mwenye tamaa ya mali; huuondoa uhai wao walio nayo.*"

Hiyo ndio njia ya tamaa; huangamiza wale walio nayo.

Wakati ambapo mfano katika kifungu chetu cha maandiko linahusu mauaji na ujambazi, mfumo hushikilia kweli kwa tabia zote za dhambi. Sasa ebu na tupanue somo la kujifunza hapa.

Hatari Ya Marafiki Waovu

Hushawishi kupitia vishawishi

Kama nyoka aliyemjaribu Hawa, marafiki wenye dhambi wataenda katika:

- Tamaa ya mwili ("nzuri kwa chakula").
- Tamaa ya macho ("hupendeza macho").
- Kiburi cha uzima ("humfanya mtu kuwa mwerevu").

Kama katika Mwanzo 3:6, "*Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti <u>wafaa kwa chakula</u>, <u>wapendeza macho</u> nao ni mti wa <u>kutamanika kwa maarifa</u>, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe naye akala.*"

Marafiki waovu watatoa taraja rahisi; kama vile mali bila kufanya kazi; kama vile starehe pasipo kuwajibika; kama vile urafiki pasipo gharama.

Inasikika vizuri na rahisi, siyo?

Wanakataa gharama ya dhambi; kwamba dhambi huwaangamiza wale walio nayo

Wanaojiita "marafiki" watawageukia mmoja baada ya mwingine. Kama watatenda dhambi pamoja nawe, unajuaje kama hawawezi kufanya dhambi dhidi yako? (kama kundi la mbwa). Watakuwa marafiki pale tu inapowafaidisha wenyewe.

Kwamba dhambi huwaingiza wale wanaoendelea nayo.

Hesabu 32:23, "*Lakini kama hamtaki kufanya neno hilo, ninyi mmefanya dhambi mbele za BWANA nanyi jueni ya kwamba hiyo dhambi yenu itawapata hapana budi.*"

Dhambi inahitaji uongo na udanganyifu; ghafla mtu anajikuta akikamatwa katika kundi la uongo.

Mara nyingi dhambi huchukua gharama ya kimwili ambayo haiwezi kufichika.

- Ulevi (dawa za kulevya).
- Ugonjwa.
- Mimba zisizo tarajiwa.

Marafiki waovu hawazungumzii ghara ya dhambi, au sivyo?

Mwisho, tutoke katika kifungu chetu je ni nini…

Suluhisho La Marafiki Waovu

Usiwasikilize

Mith. 1:10, "*Mwanangu wenye dhambi wakikushawishi, wewe usikubali.*"

Wanachokiahidi hawawezi kukitoa, angalau kwa muda mrefu.

Mtu mwema aliyebarikiwa hatembei katika shauri lao. Zaburi 1:1, "*Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mizaha.*"

Kuwa mwerevu vya kutosha usisikilize maneno yao yenye vishawishi.

Kaa mbali nao

Mith. 1:15, "*Mwanangu usiende njiani pamoja nao; uzuie mguu wako usiende katika mapito yao.*"

Usiwaruhusu wawe marafiki zako. Mith. 13:20, "*Enenda pamoja na wenye hekima, nawe utakuwa na hekima; bali rafiki wa wapumbavu ataumia.*"

Hasa kama siyo waamini. 2 Kor. 6:14-18, "*Msifungiwe nira pamoja na wao wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza? Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja nay eye asiyeamini? Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema ya kwamba, nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Kwa hiyo tokeni kati yao, mkatengwe nao asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi.*"

Kuwa mwerevu kuwaepuka wasiwe marafiki zako.

Hitimisho

Hii siyo kusema kwamba hatupaswi kujaribu kuwaokoa.

Tunapaswa kutengwa na dunia, bali hatuwezi kujitenga wenyewe.

1 Kor. 5:9-11, "*Naliwaandikia katika waraka wangu, kwamba msichangamane na wazinzi. Sisemi msichangamane kabisa na wazinzi wa dunia hii, au na wenye kutamani, au na wanyang'anyi, au na wenye kuabudu sanamu; maana hapo ingewalazimu kutoka katika dunia. Lakini mambo yalivyo, naliwaandikia kwamba msichangamane na mtu aitwaye ndugu, akiwa ni mzinzi au mwenye kutamani au mwenye kuabudu sanamu au mtukanaji au mlevi au mnyang'anyi; mtu wa namna hii msikubali hata kula naye.*"

Yesu alipokuwa na wenye dhambi. Mat. 11:19, "*Mwana wa Adamu alikuja akila na kunywa, wakasema, mlafi huyu, na mlevi, rafiki yao watoza ushuru na wenye dhambi! Na hekima imejulikana kuwa ina haki kwa kazi zake.*"

Alikuwa nao akiwafundisha, lakini hakushiriki katika matendo yao maovu.

Lakini tunapaswa kuwa wakweli sisi wenyewe. Je tunawavutia sana kuliko wanavyotuvutia? Kama sivyo, basi tunapaswa kukaa mbali nao hadi wakati ule tutakapo pata nguvu.

Tulichojifunza katika Mithali 1:10-19, labda, tunaweza kuiweka katika mkhutasari na mtume Paulo: 1 Kor. 15:33, "*Msidanganyike, mazungumzo mabaya huaribu tabia njema.*"

Kuwa mwerevu, tunapaswa kutambua nia nani tumsikilize (Mungu, wazazi, na marafiki wema), na hatupaswi kumsikiliza nani (mtu ye yote anayetuvutia katika kutenda uovu).